Research Journal in African Languages
https://royalliteglobal.com/african-languages

African Languages




Research Article

*Section:* Languages

Check for updates

This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in African Languages*, Volume 2, Issue 2, 2021

**Article Information**
Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th May 2021
Published: 18th June 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# Identifying and use of imagery in selected songs of Mrisho Mpoto

**Geoffrey Mandila[1], Nilson Opande[2] & Fred Simiyu[3]**
[1,2] Department of Kiswahili and Other African Languages, Kisii University, Kenya
[3] Department of Kiswahili and Other African Languages, Kisii University, Kenya
Correspondence: jeffmandila@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-4982-5698

## Abstract

This work aims to analyse the imagery in the songs and how they are contributions in selected songs of Mrisho Mpoto. This research was led by the stylistic theory that deals with the use of words in a unique way and thus makes language difficult or easy, preventing the writers feelings that seems to be ridiculed, affectionate, optimistic, harshness or sarcasm, the use of stylistic devices such as similes, metaphor, personification among others. The selection of stylistic devices used to influence the target audience, the use of style by focusing on specific contests in story telling or telling events. However, this research focused on three main pillars; words are used artificially making the language difficult or easy, the author's feelings are evident, expressing ridicule, affection, optimism, harshness or sarcasm from the use of language; the selection of used style brings attraction to the target audience. The findings of this research reveals that the songs of Mrisho Mpoto due to the use of imagery many of their lovers do not understand them very well. So we suggested further research into this composition in the aspects of art.

**Keywords:** art, imagery, Mrisho Mpoto, song

**Public Interest Statement**

This research was led by the stylistic theory that deals with the use of words in a unique way and thus makes language difficult or easy, preventing the writers feelings that seems to be ridiculed, affectionate, optimistic, harshness or sarcasm, the use of stylistic devices such as similes, metaphor, personification among others.

**How to Cite:**
Obwoge, B. K. C. (2021). Language and power relations in gendered discourse within EkeGusii: Implications on pedagogy in the Kenyan context. *Research Journal in African Languages*, *2*(1). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/608

© 2021 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

Research Journal in African Languages
https://royalliteglobal.com/african-languages




Research Article

Section: Languages

Check for updates

This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, Volume 2, Issue 2, 2021

**Article Information**
Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th May 2021
Published: 18th June 2021

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Obwoge, B. K. C. (2021). Language and power relations in gendered discourse within EkeGusii: Implications on pedagogy in the Kenyan context. *Research Journal in African Languages*, *2*(1). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/608

# Ubainishaji na matumizi ya aina za jazanda katika nyimbo teule za Mrisho Mpoto

**Geoffrey Mandila[1], Nilson Opande[2] na Fred Simiyu[3]**
[1,2] Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kisii, Kenya
[3] Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya
Correspondence: jeffmandila@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-4982-5698

**Ikisiri**
Tasnifu hii inalenga kushughulikia nyimbo teule za Mrisho Mpoto. Imeshughulikia jazanda katika nyimbo hizi kwa kutumia nadharia ya kimtindo. Kazi hii inadhamiria kuchanganua jazanda katika nyimbo za Mpoto na jinsi ambavyo jazanda hizo zinachangia kuwasilisha maudhui katika nyimbo hizo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kimtindo ambayo inahusu matumizi ya maneno kisanaa hivyo basi kuifanya lugha kuwa ngumu au rahisi, kuzua hisia za mwandishi zinaonekana, zikionyesha dhihaka, mapenzi, matumaini, ukali au kejeli, matumizi ya tamathali za usemi kama vile tashbihi, sitiari, tashihisi na kadhalika kwa wingi, uteuzi wa msamiati uliotumika huleta mvuto kwa hadhira lengwa, matumizi ya lugha kwa kujikita katika miktadha maalumu katika kusimulia hadithi au kueleza matukio. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika mihimi mitatu mikuu; maneno hutumiwa kisanaa hivyo basi kuifanya lugha kuwa ngumu au rahisi; hisia za mwandishi zinaonekana, zikionyesha dhihaka, mapenzi, matumaini, ukali au kejeli kutokana na matumizi ya lugha; uteuzi wa msamiati uliotumika huleta mvuto kwa hadhira lengwa. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa nyimbo za Mrisho Mpoto kutokana na matumizi ya jazanda, wapenzi wake wengi hawazielezi vyema. Hivyo basi tukapendekeza tafiti zaidi kufanywa katika nyimbo hizi katika vipengele vingine vya kisanaa.

**Maneno muhimu**: jazanda, sanaa, Mrisho Mpoto, nyimbo

## 1.0 Utangulizi

### 1.1 Maisha ya Mrisho Mpoto

Mrisho Mpoto alizaliwa mnamo tarehe 7 Oktoba, 1978 mkoani Ruvuma katika wilaya ya Songea katika taifa la Tanzania. Kiasili, Mrisho Mpoto ni Mngoni kutoka kaskazini mwa jamhuri ya Tanzania. Ni mtoto wa kumi na mbili kwa mke wa kumi na mbili ambaye ndiye aliyekuwa mke wa mwisho wa *Mzee Chifu Mpoto*. Katika familia nzima, Mrisho ni mtoto wa thelethini na sita ambaye pia ndiye wa mwisho kwa aila yao. Kule kwao Songea, yeye hujulikana kama "*Mrisho Mpoto wa Mwisho*." Kuhusu elimu, Mrisho hakupata masomo ya kiwango cha juu maana hakuingia sekondari maana ni mhitimu wa darasa la saba ambalo kulingana naye mwenyewe alipokuwa akihojiwa na mwanahabari wa *Cloud Media Studio,* alidai kuwa alifeli mtihani wake. Mwanamuziki huyu alikiri hadharani kuwa maishani hakuwa na matumaini wala dira kutokana na ukubwa wa familia yake uliyokuwa kizuizi kikubwa kwa wazazi wake kumkimu namna watoto wengine walivyokuwa wakikimwa.

### 1.2 Jazanda inavyojitokeza katika nyimbo teule

Nyimbo za Mrisho Mpoto zimesheheni jazanda ambayo ni mbinu ya uwasilishaji ujumbe ambapo mwandishi na au msemaji hutumia mafumbo ya kiistiari kuelezea mambo yaliyofichika. Katika uchambuzi huu, utafiti huu ulijikita katika nadharia ya kimtindo katika ufafanuzi wa jazanda katika nyimbo hii. Katika ilivyoelezwa katika nadharia, mtindo humtambulisha mtu kutokana na semi zake. Hivi, kupitia nadhari hii, inakuwa rahisi kutambua maana inayojitokeza katika nyimbo za mwanamuziki huyu. Hali hii humfanya msikilizaji kusalia katika wingi wa fikra za kutaka kufahamu zaidi. Katika nyimbo zake teule, Mrisho Mpoto ametumia jazanda namna ifuatavyo:

**Ndoto-** Kauli hii alitumia kijazanda kuelezea kuhusiana na hali ya kumwelezea mwenzio mambo ambayo hayana umuhimu wowote kwake huku ukificha yale yenye umuhimu mkuu. Kwa kawaida, ndoto ni jambo ama mambo ambayo mwanadamu hupitia na kuyafanya akiwa usingizini. Wakati mwingine ndoto huhusisha mazungumzo na matendo. Hata hivyo, katika utunzi huu, Mpoto alikuwa akiionyo jamii dhidi ya kujishughulisha na mambo yasiokuwa maana kwao. Anatoa mafunzo kwa wasikilizaji wake wawe wale wanaotoa ahadi ambazo zinaweza kutimizwa wala sio ahadi zinazoonekana kama ndoto ambayo haziwezi kutimilika.

**Wakati-** Hapa, mwanamuziki huyu alikuwa akijaribu kuwahimiza watu na jamii kwa ujumala kuhusiana na umwafaka katika muda. Kulingana na kamusi elezi (2016) wakati ni kipindi, msimu, muda ama majira fulani. Kulingana na Mrisho Mpoto, hataki watu wawe wa kupoteza muda mwingi maana muda huo unapoenda, katu hauwezi kurejea tena. Alikuwa anawahimiza kuhusiana na uongozi wa awamu mbalimbali wa Tanzania ulio wenye matarajio, ubarakala na awamu ya kuogopa lawama na kutimiza ahadi zao kulingana na muda uliopo.

**Ukuta-** Kulingana na utafiti, ilibaini kuwa Mpoto anaamini kuwa chochote kile kinachozuia maendeleo katika jamii, ni ukuta. Mpoto anaamini kuwa ukutu ni kizuizi cha mwangaza ambao wananchi wanafaa kuupata. Kimaana, ukuta ni kizuizi kilichojengwa kwa mawe ama tofali. Hivi, katika wimbo huu, Mpoto alikuwa akiwahimiza viongozi

dhidi ya kuweka vizuizi mbele katika juhudi zao za maendeleo. Mwanamuzi huyu alikuwa akiwahimiza viongozo kuwa wenye uwazi ili kuafikia ndoto zao za maendeleo.

**Paka-** Hapa, mwanamuziki huyu alikuwa akijaribu kuwatahadharisha watu kuwa makini punde waonapo dalili ya hatari na mambo kutendeka kinyuma na matarajio basi kuna kila sababu ya kutahadhari. Kungana na tamaduni za Kaifrika, jamii nyingi zimehusisha paka na mikosi ama mambo ya kishetani. Hivi, mwanamuziki huyu alikuwa akiwahimiza mno wasikilizaji wake kuwa tahadhari na mienendo ya kiongozi wao hasa wanapoona paka kalala chali maana ndio mwanzo wa kisirani.

**Bidhaa-** Neno hili limetumiwa kumaanisha wanawake wanaondesha biashara za kimapenzi. Kulingana na mwanamuziki huyu, wasichana wadogo wanafanya mapenzi kutokana na ugumu wa maisha wanayoyapitia. Awamu mbalimbali za uongozi katika taifa la Tanzania zimewafanya watu kusalia maskini na kuendesha biashara za ukahaba ili kuyakidhi maslahi yao. Kuwalinganisha wananchi na bidhaa ni jazanda ambayo ilikuwa inawazindua viongozi kuhakikisha kuwa wanatoa hudumu nzuri kwa wananchi ili maisha yawe yenye maadili mema.

**Mgongo-** Mwanamuziki huyu alikusudia kuelezea kuhusu maovu ambayo yalikuwa yametendewa jamii. Kulingana na utafiti huu, ilibainika kuwa Mpoto alikuwa akiwahimiza Watanzania wageuke na kuyapa mgongo yaliyopita na kuyaacha kuwa historia. Kulingana na utafiti wetu, mwanamuziki huyu alikuwa akilia maridhiano yawepo ili jamii iweze kutangamana upya kwa kusahau yaliyokuwa yamepita.

**Mbwa-** Utafiti wetu ulibaini kuwa kutokana na ugumu wa maisha katika bara la Afrika, mwanamuziki huyu anachekesha kwa kutumia jazanda kwa kudai kuwa ni vyema kuwa mbwa Ulaya kuliko kuwa mwana wannchi. Japo inaonekana dhihaka, mwanamuziki huyu alikuwa akitilia mkazo swala la ugumu wa maisha ambao limeruhusiwa kujipenyeza katika jamii kutokana na uwamu mbalimbali za uongoz ambao uliwapotosha wananchi.

**Milango-** anamuziki ametumia neno hili kumaanisha njia halali ya kutendea jambo. Anamhimiza kiongozi wa awamu ya matumaini kuwa kiongozi anayefuata kanuni na kufuata njia halali za kupata ufanisi. Kulingana na maelezo ya Kamuzi Elezi (2016) mlango ni uwazi ulio ukutani mwa kitu kama vile nyumba ambao hurusu watu kuingia ndani na kutoka. Ila kulingana na utafiti huu, ilibaini kuwa viongozi wengi walikuwa wakitumia maeneo yasiyofaa kujipenyeza ndani. Maeneo hayo yasiyofaa ndio njia za mkato ambazo Mrisho Mpoto anazikashuif katika juhudi za viongozi wanapokuwa mamlakani.

**Dirisha-** Ni neno la kijazanda ambalo mwanamuziki huyu ametumia kumaanisha njia haramu za kimkato za kufanya jambo. Kilingana na mwanamuziki huyu, anamwonya kiongozi wa awamu ya sasa yenye matumaini kuwa makini na kuepuka njia haramu za kujiatia mali. Anahiiza viongozi kuingia ndani kwa kutumia mlango (kutumia njia halali) wala wasitumie madirisha (njia za mikato kujipatia nafasi. Kulingana na utafiti huu, ilibainikuwa kuwa mwanamuziki huyu alikuwa akiimiza maadili kuzingatiwa katika uongozi.

**Baraza -** Kulingana na utafiti wetu, ilibainika kuwa mwanamuziki huyu alitumia neno hili kijazanda. Kuwa baraza kwa kawaida huwa ni mahali pa mkutano unaolenga kutatua hali fulani, lakini katika *Sizonje*, barazani imetumiwa kama eneo ambalo watu hutulia kwa nia ya kupata kujua yanayoendelea ndani ya jengo au taasisi fulani. Ndiposa anasema kuwa

*walikaa hapo wakasikia kelele kutoka ndani*. Kiini cha kuketi barazani kilikuwa kuyasikiliza maovu ambayo viongozi walikuwa wakiyaendeleza mle ndani ambayo kwa kiasi fulani hayakuwaridhisha. Mrisho Mpoto anasema kuwa *walisikia mtu akiruka dirishani*.

Yapo matumizi mengine ya jazanda katika huu wimbo wa *Sizonje* pale mwanamuziki huyu anapotumia neno *mundu*. Kulingana na utafiti wetu, mwandishi alitumia jazanda hii kwa ishara ya *kadi ya kura*. Ilibainika kuwa anasema, *"Hii ndiyo nyumba yetu tulipoficha mundu za kupondea wezi."* Kwamba, sila ya kuwaondoa viongozi wabaya kwenye mamlaka ni kadi ya kura. Papo hapo, ametumia jazanda ya *wezi* kumaanisha viongozi walio na uchu na ashiki ya kuwachukulia wananchi mali pasipokuwa na idhini. Mwanamuzi huyu anawataja na kuwalinganisha viongozi hawa na wezi ambao wanafaa kuangamizwa na silaha ya mundu. Ilivyo katika nyimbo nyinginezo, wimbo wa *Kitendawili* umesheheni misemo yenye wingi wa jazanda kiwango cha kumtatiza msikilizaji. Katika hali hii, hapa ni baadhi tu ya kauli zake zenye kuwa na maana fiche.

**Kuku**- Jazanda hii imejitokeza mwanzoni mwa wimbo huu. Katika sura ya nje, ni bayana kuwa kuku anayetaga mayai hafai kuchinjwa kutokana na umuhimu wake hasa kwa yale mayai na vifaranga wanaotayajiwa. Huu ni uhasilisia, lakini katika wimbo wa Mrisho Mpoto ambayo kwa hakika umeimbwa katika awamu ya uongozi wa rais wa sasa Mheshimiwa John Pombe Mogofuli, jazanda hii ilikuwa inakosoa uongozi wake ambao ulikuwa unawashambulia wateka uchumi katika taifa la Tanzania. Ni kipindi ambacho uongozi wa jamhuri ya Tanzania ulikuwa unawahamisha watu waliokuwa wakitoka mataifa ya nje kwa misingi kuwa wanamiliki mali nyingi katika uchumi wa taifa la Tanzania. Hivyo, mwimbaji huyu alikuwa anaijuza serikali kuhusiana na hasara ambayo ingepata iwapo wawekezaji hawa aliowalinganisha na kuku mtaga mayai wangeondolewa.

**Sizonje**- Ni jazanda nyingine pale ambapo mwimbaji anarejelea wimbo wake wa awali wa Sizonje. Anadai kuwa katika Sizonje, alimuita aingie ndani. Ila kule kuingia ndani kulikuwa na sheria zake. Mwimbaji anamkumbusha kuwa kila anayeingia ndani hutoka. Jazanda hii bado inagusia utawala wa kiongozi wa sasa John Pombe ambaye anakumbusha kufuata sheria katika uongozi wake. Kutokatalia katika uongozi ambao wananchi ndio wamempa.

*Nilikuita sizonje ili uingie ndani*
*Kwa sababu kila anayeingia lazima atoke nje*

**Masomo**- Walisoma hapa, walimaliza hapa kila kitu kiliishia hapa. Jazanda hii katika wimbo wa Kitendawili inaonyesha matumizi mabaya ya mamlaka. Mwimbaji anamkumbusha kiongozi wake kuhusiana na watangulizi wake ambao walipoingia mamalakani, walifanya kila mbinu kuhakikisha kuwa wanawafilisi wananchi kwa kutumia kauli hizi hapa. Anawahimizi viongozi wa sasa kupata mafunzo kutokana na awamu zilizotangu ambazo zilijikusanyia rasilimali zote na kuwaacha wananchi katika hali mbaya ya kimaisha.

**Nyama**- Utafiti huu ulibaini kuwa Mrisho Mpoto alizua suala ambalo linaigusa jamii moja kwa moja. Mpoto ametumia jazanda ya nyama kuonyesha jinsi ambavyo viongozi

wanapata mali na uwezo mkubwa huku wakiwaacha wananchi katika hali ya umaskini mkubwa. Anasema kuwa viongozi wanakula nyama wakiwaachia wananchi mifupa ambayo haina minofu. Mpoto anawahimiza viongozi kuepukana na uongozi wa kuwadhalalisha na kuwanyanyasa wanyonge ambao kila wakati wamesalia kuwa taabani.

**Kifo**- Mwimbaji anafichua maumivu wanayopata wananchi katika utawala wa taifa la Tanzania. Anasema kuwa kuna baadhi ya wananchi ambao hawaridhiki na uongozi uliopo kiwango kuwa wanaumia kimya kimya. Ila, kuna wale ambao wamejitokeza kuwa kulalamika hadharani hadi vilio vyao vinasikika moja kwa moja. Kulingana na mwimbaji huyu, makundi haya yote mawili yanalilia uongozi mmoja ambao upo hatamuni. Anasema kuwa wao wanafariki kifo ambacho kwa hakina kinaweza kukigika awapo wananchi wanajifunza kuchagua viongozi ambao wanastahili kuwaongoza.

*Wapo wanaolia kwa kuhisi wamedanganywa*
*Wapo wanaolia kupoteza ndugu zao*
*Lakina wapo wanaolia kuona kuna msiba kwao*
*Lakini marehemu ndio mwandaaji…*

**Mifupa -** Kuhusu ugavi wa pato la nchi pia ni suala ambao Mpoto amelingazia kwa kina mno kwenye wimbo wake wa Kitendawili. Analalamika kuwa kuna wale wanaopata zaidi ya wingi licha yao kuwa katika kiwango kimoja. Analinganisha hali hii na sherehe ambao wengine hula mnofu wa nyama huku wengine wakipewa mifupa kwa wale mweupe.

*Wali mweupe kwa shekheee,*
*Watoto kaeni wanne wanneeee,*
*Waandaaji tutakula uwani tena mwishoo.!*

Hizi ni baadhi tu ya jazanda katika wimbo wa Kitendawili ambao kwa hakika ni wimbo ambao umeimbwa katika awamu iliyopo ya uongozi wa jamhuri ya Tanzania. Jazanda ikiwa mbinutawala katika nyimbo za Mrisho Mpoto, mwanamuziki huyu ameitumia vile vile anaposema kuwa ukutani palikuwapo na *picha.*

**Picha**- imetumiwa kijazanda. Analelezea kuhusu picha mbili ambapo moja ni picha na nyingine ni mchoro wa picha ya kwanza. Picha hizi zote mbili zinaonyesha urithi katika uongozi wa taifa. Kwamba, viongozi wetu hawana mapya ya kuwapa wananchi mbali na kuzifuata nyayo za viongozi wa awali ambao kwa njia moja au nyingine, hawajawafanyia wananchi lolote la shukrani. Mwanamuziki huyu anawalinganisha viongozi hao na picha zilizotundikwa ukutani ambazo hazina manufaa yoyote. Jazanda ya picha inatupa taswira njinsi ambavyo utendakazi wa viongozi wetu ulivyo.

**Wimbo**- Ilibainika kuwa mwanamuziki huyu alikuwa na maana fiche aliposema kuwa wimbo mbaya haufai kumbembelezea mtoto. Katika utafiti wetu, jazanda iliyokuwa hapa ni *wimbo.* Neno hili limetumiwa kwa misingi ya huduma. Mwanamuziki huyu alimaanisha kuwa huduma ambayo haifai, haistahili kutumiwa kwa manufaa ya wananchi. Kwake Mrisho Mpoto anaonekana kuukosoa vikali mno uongozi ambao kamwa hautilii kipaumbele

maslahi ya wananchi. Anaafadhalisha mbinu mbadala itumiwe kuliko kuendelea kuwa na viongozi wasiojua kuwajibika.

**Bahasha-** utafiti wetu ulibaini kuwa mwanamuziki huyu alitumia maneno *bahasha za khaki* kijazanda. Tulibaini kuwa maneno haya yalikuwa na maana fiche ya ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana. Ukosufu wa kazi ndio ulisababisha uwepo wa maandamano yanayoupinga uongozi uliojaa uchu wa mali kwa kupitia njia ya mkato. Hili lilibainika wazi pale ambao maneno mateule ambayo Mpoto anayatumia kwa kuwaelezea vijana wenye bahasha mikononi, yanadhihirisha hisia za huruma.

## 2.0 **Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti (Literature Review)**

### 2.1 Matumizi ya jazanda katika nyimbo

Kwa mujibu wa Crystal na Davy (1969) umtindo una dhima ya kuchanganua tabia za lugha kwa lengo la kubainisha sifa mahususi ambazo zimejikita katika miktadha maalumu kutokana na sifa za sifa za kijumla za kiisimu. Tofauti na utafiti huu, utafiti wetu unalenga kuonyesha ni kwa jinsi ganijazanda imesawiriwa kama chombo cha kipekee ambacho Mrisho Mpoto amekitumia kuisuta jamii kwa kutumia meneno yenye hisia mbalimbali. Katika nyimbo zake zote ambazo tuliziteua, mwanamuziki huyu alionekana kuimba nyimbo zake kwa lengo la kuificha jamii kile alichokuwa akikiimba.

Kwa mujibu wa Finnegan (1977) nyimbo ni chombo mwafaka cha fasihi simulizi ambacho huiongoza jamii kufanikisha malengo yake. Hivyo basi, nyimbo huwa na dhima ya kuelimisha, kuburudisha na kuonya jamii husika. Njia mojawapo ambayo nyimbo hutekeleza dhima ya kuelimisha, kuburudisha na kuonya ni kupitia matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi, mojawapo ya tamathali hizo ikiwa ni matumizi ya jazanda ambayo anaitumia Mrisho Mpoto kuelimisha na kuikosoa jamii kupitia jazanda ambazo anazitumia kimtindo. Mbinu hii japo inawasumbua wengi kuelewa, imefaulu kuikosoa kisiasa, kitamaduni na kiuchumi.

Lawal (1997) anafafanua mbinu ya mtindo kama chombo cha lugha ambacho hushughulikia upekee lugha iyo hiyo kwa kauli na kuihamasisha na dhana kupitia kwa uteuzi wa maneno maalumu yenye hisia mbalimbali. Leech na Short (2007.9) wakatoa maoni yao yaliyobaini kuwa mbinu ya mtindo ni kipengele cha lugha ambacho hulenga wazo husika moja kwa moja kutokana na upekee wa lugha tumizi kwenye fasihi kwa dhana ya hisia mbalimbali. Tofauti iliyobainika kutokana na michango hii ya kifasihi ya wasomi hawa kuhusu wazo moja la mbinu ya kimtindo inategemea kile walicholenga kuwasilisha, ila hatima yao ilikuwa moja kwamba, upekee wa matumizi ya lugha yenye hisia humtambulisha mwanasanaa. Nordquist (2015) alichangia maoni yake pia kuhusu mtindo ambapo alisema kuwa ni kiungo muhimu cha sanaa chenye upekee fulani wa kumtambulisha mwanasana kutokana na fikra na mtindo wa uwasilishaji ujumbe. Mara nyingi, utamtambua mwanasana kutokana na mpangilio wa kimtindo wa kazi yake na nia anayodhamiria katika jamii.

Naye Wamitila (2003), anadai kuwa dhana ya mtindo huelezea jinsi ambavyo msanii mwenyewe anavyojieleza. Kuwa tunaweza kueleza mtindo namna ambavyo msanii mwenyewe anavyojieleza katika sanaa yake. Anasema kuwa mtindo hushughulikia uteuzi binafsi wa tamathali za kifasihi. Sawa na utafiti wetu, tuligundua kuwa jazanda humhusu

na kumtambulisha msanii kutokana na hisia ambazo huibua wakati wa uwasiliaji wake wa malengo. Jazanda anayoitumia Mrisho Mpoto humtofautisha na wanasanaa wengine wote kuwa mwenye upekee wa aina yake.

Malenya (2008) ametafitia matumizi ya lugha na jazanda katika nyimbo za Jacob Luseno kwa kutumia nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Alionyesha jinsi Luseno alivyoteua tamathali za usemi katika vipindi vitatu vya utawala nchini Kenya na jinsi lugha ilivyooana na matukio mbalimbali nyakati hizo. Aligundua kuwa lugha na jazanda alizotumia Luseno ziliafikiana na matukio katika vipindi vyote vya utawala nchini Kenya. Utafiti huu unakaribiana sana na wetu hivyo basi utatufaa sana katika kuangazia kipengele cha jazanda. Tofauti zilizopo baina tafiti hizi mbili ni kuwa, nyimbo za Luseno zinaangazia mazingira na utamaduni wa jamii ya Waluhya nchini Kenya ilhali za Mrisho Mpoto ni za lugha ya Kiswahili na zimeangazia sana utamaduni wa nchi ya Tanzania.

Kwa upande wake Swaleh (2011), alifanya utafiti wa maumbo na mitindo iliyosheheni katika Usawiri wa Uana na Mamlaka kuwa mfumo maalumu wa kuelezeka. Anadai kwamba msanii huwa na uhusiano wa moja kwa moja na sanaa yake na kumtambulisha. Mawazo yake yana mashiko maana anadai kuwa mtindo ndio huwa kitambulisho cha sanaa na msanii. Hata hivyo, Swale alikuwa akizungumzia tamathali zote za kisanaa ila utafiti wetu ulijikita katika mtindo wa jazanda peke yake ambao kwa kiasi kikubwa unamtambulisha Mpoto katika jamii. Swala hili zimebainika kutokana na jazanda zake katika nyimbo teule ambazo zinafanya nyimbo hizi kuwa zenye upekee fulani katika jamii na kuzua hitaji la kuwepo kwa haja ya kuzichanganua.

Mungai (2014) ametafiti kuhusu fani katika nyimbo teule za Anastacia Mukabwa. Alibaini kwamba nyimbo za anastacia Mukabwa zina ukwasi wa fani kama vile wahusika, maudhui, mandhari, toni, tamathali za usemi, sitiari, ishara, umbo na mtindo. Ijapokuwa utafiti huu unatofautiana na wetu kwa sababu umeangazia kipengele cha fani kwa jumla, utatufaidi kwa kuwa umerejelea kipengele cha jazanda.

Alifah (2015) alichunguza aina mbalimbali za mbinu za lugha katika nyimbo teule za Michael Jackson na akabaini mbinu 11, mojawapo ikiwa ni jazanda. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu umeshughulikia nyimbo katika utamaduni tofauti na pia kipengele cha jazanda kimegusiwa tu. Tutafaidika kutokana na utafiti huu kwa kurejelea kipengele cha jazanda ambacho kimetumiwa kama mojawapo ya mbinu za lugha.

Putra (2017) alichanganua mbinu za lugha katika beni ya Scorpions kwa kutumia nadharia ya Lyon ambapo alibaini kuwa nyimbo za beni ya Scorpions zina ukwasi mkubwa wa mbinu za lugha. Baadhi ya mbinu hizi ni pamoja na tashbihi, istiari, kinaya, jazanda, uhuishi, chuku, vinyume na kadhalika. Anaendelea kueleza kwamba matumizi ya mbinu za lugha katika nyimbo hupendeza na kuongeza ujumi. Ijapokuwa utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa umeangazia mbinu nyingi za lugha kwa pamoja na pia unalenga wasanii tofauti, utatufaa kwa sababu umeangazia kipengele cha jazanda ingawa kwa ufinyu.

### 1.2 **Jinsi jazanda hupelekea kuibuka kwa maudhui**

Lodge (1972) anaelezea kuwa mtindo ni jinsi ya kujieleza. Mtunzi anayaeleza mambo ya kawaida kisanaa ili yalete maana ya undani. Anaendelea kusema kwamba mtindo ni mtu

yaani kila msanii ana mtindo wake unaomtambulisha. Kwa mujibu wa maelezo haya ya Lodge, Mrisho Mpoto anatambulishwa kwa matumizi ya jazanda yenye kina katika utunzi wa nyimbo zake, jambo linalomtofautisha na watunzi wengine wa nyimbo za densi. Nyimbo zake zinadhihirisha ufundi mkubwa kwa sababu ametumia jazanda kuibua masuala mazito ya kijamii. Matumizi hayo ya jazanda pia yamedhamiriwa kuwahamasisha na kuwasisimua wasikilizaji wake.

Leech na Short (1981) wanafafanua mtindo kama namna ambavyo mtu huitumia lugha kama mali yake binafsi. Aidha, mtindo ni jinsi ambavyo msanii huiteua lugha ili kuitumia katika kazi ya sanaa. Jinsi mtunzi wa kazi ya fasihi anavyoteua msamiati, jazanda, tamathali za usemi na miundo ya sentensi huishia kumpa utambulisho. Kulingana na msomi Ntaragwi (1990) alibainisha jinsi nyimbo za Ramadhani Ogalla zinavyoleta maudhui ya utetezi wa wanyonge. Maudhui katika nyimbo za Ramadhan zililenga kuwatetea watu wa Afrika Mashariki ilhali utafiti wetu ulilenga nyimbo za Mrisho Mpoto ambapo jazanda yake ililenga kuonyesha maisha ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni katika awamu mbalimbali katika serikali za jamhuri ya Tanzania tukijihusisha na nadharia ya kimtindo.

Yalwala (1991) alifanya uchunguzi wa maudhui katika nyimbo za John Mwale ambapo alijikita katika maudhui ya ya kijamii. Utafiti huo ulichanganua maudhui mbalimbali kwa kutumia muktadha wa mazingira. Hata hivyo, tofauti na utafiti huo, utafiti wetu ulilenga kuchanganua namna ambavyo jamii imeathirika kichanya na kihasi kutokana na jazanda iliyojikita katika nyimbo za Mrisho Mpoto huku tukujikita katika nadharia ya kimtindo.

Nkongwe (1988) naye alitafiti mbinu tofautitofauti na maudhui katika nyimbo za mwanamuziki Joseph Kamaru. Utafiti huo ulionyesha namna ambavyo Kimaro alionyesha maudhui mbalimbali ya kijamii na kisiasa nchini Kenya. Kazi hii japo haipo sawa na kazi yetu, sisi tulitafiti matumizi ya jazanda katika awamu mbalimbali za uogozi wa kisiasa na kijamii katika taifa la Tanzania. King'ei (1992) naye alifanya utafiti kuhusu lugha na utamaduni katika nyimbo za taarab kati ya miaka ya 1963-1990. King'ei aligundua kuwa nyimbo za taarab ziliendeleza utamaduni kupitia maudhui yake kwenye jamii za watu wa ukanda wa Afrika Mashariki. Tofauti na tasnifu yake, yetu ilikusudia kuangazia namna ambavyo jazanda katika nyimbo za Mriso Mpoto zilivyoendeza maudhui ya utamaduni.

Kieti (1989) alichanganua taswira na mazingaombwe nyimbo kwa ujumala. Alibainika kuwa wengi wa wanamuziki hutumia taswira kuwasilishha ujumbe katika mazingira ya miujizamiujiza. Aligundua kuwa baadhi ya majina wanayoyatumia yana maana fiche ambayo haileweki moja kwa moja. Sawa na utafiti wetu, tulibaini kuwa mbinu ambayo Mrisho Mpoto aliitumia kuwasilishia maudhui yake yalikuwa fiche ambayo hayakuwa yakijitokeza moja kwa moja.

Haynes (1995) anasema mtindo ni uchunguzi wa makini wa maneno katika matini unaozingatia jinsi tunavyoangalia tunachozungumza au tunachoandika. Mtindo pia ni mpangilio wa ruwaza za matini kwa ujumla. Maoni yake ni kuwepo kwa uchunguzi makini wa maneno katika utunzi na ruwaza za matini. Maoni yake yanawiana na utafiti huu kwa sababu utunzi wa Mrisho Mpoto una sifa za kimtindo zinazohusiana na uteuzi wake wa makini wa maneno ili yawiane na dhamira yake.

Omwoyo (1997), alishughulikia fani katika bahari ya mashairi ya Hassan Mwalimu

Mbega. Alichanganua diwani ya Dafina ya Malenga. Alitumia nadharia ya urasimu katika utafiti wake. Utafiti wake ulionyesha kuwa, fani ina mchango mkubwa katika ufumbata wa dhamira ya mtunzi. Alisema kuwa fani ni kipengele muhimu cha fasihi. Tofauti na utafiti wake, tulilenga uhakiki wa mbinu ya jazanda katika nyimbo teule za msanii Mrisho Mpoto na namna amabyo jazanda hii imepekea uwepo wa maudhui. Katika uchanganuzi wetu, tulibaini kuwa jazanda ina mchango mkubwa sana katika ujenzi wa maudhui yanayoonesha vipindi mbalimbali vya uongozi katika tiafa la Tanzania.

Wambua (2001) ameshughulikia mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alichunguza namna matumizi ya tamathali za usemi yanavyosaidia kupitisha maudhui kwa walengwa. Japo utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu umeangazia nyimbo katika jamii ya Wakamba, tutafaidika kwa kurejelea kipengele cha jazanda katika nyimbo teule za Mrisho Mpoto.

Kovecses (2002) anasema kuwa maudhui huweza kutumiwa kijazanda kwa nia ya kuleta mvuto katika kazi ya sanaa kutokana na matumizi ya maneno mateule yenye kubeba hisia za furaha na huzuni. Anaendelea kueleza kuwa, iwapo tunazungumza na kuandika kijazanda basi tunakusudia kuibua mvuto kwa maneno yenye ujumi au kuzua hisia kubwa. Maoni haya yanaafikiana na utafiti wetu kwa kuwa Mrisho Mpoto ametumia jazanda kiufundi katika nyimbo zake ili kuibua ujumi na kupitisha ujumbe muhimu kwa hadhira yake. Rajwayi (2009) alitafiti kuhusu maudhui na mtindo katika nyimbo za msanii Faustin Munishi kwa kutumia nadharia ya theolojia kombozi na mtindo. Utafiti ni tofauti na wetu kwa sababu umeangazia maudhui na mtindo kwa jumla japo tutafaidika kwa kurejelea jazanda kama mojawapo ya tamathali za usemi alizoziangazia mtafiti.

Kasau (2013) ameshughulikia maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za injili za Rose Muhando ambapo ameonyesha jinsi matumizi ya tamathali za usemi yalivyochangia katika ukuzaji wa maudhui. Miongoni mwa tamathali alizoziangazia ni pamoja na tashbihi, takriri, tashihisi, taashira, misemo, kinaya, sitiari, chuku na jazanda. Tutanufaika kutokana na utafiti kwa sababu ya kipengele cha jazanda kilichoangaziwa ingawa utafiti wenyewe ni tofauti na wetu kwa kuwa umeangazia maudhui na matumizi ya lugha kwa jumla. Aidha, nyimbo za Muhando zinaangazia masuala ya injili ilhali Mrisho Mpoto anashughulikia masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

## 3.0 Mbinu na Muundo wa Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na muundo wa utafiti wa kimaelezo. Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza kuwa maelezo hufafanua sampuli na pia huwasilisha data kwa kimuhtasari. Muundo huu ulitumiwa katika utafiti huu kwa kuwa utafiti huu unajikita sana katika kutoa maelezo ili kuweka bayana matokeo ya utafiti. Kothari (2007) anaeleza kuwa mbinu hii ni nzuri ya kukusanya data ambayo huhusu ufafanuzi wa sifa fulani za watu, matendo ya watu, hali ya watu au matarajio yao.

### 1.1 Mbinu za Ukusanyaji Data na Vifaa vya Utafiti

Data ya utafiti huu imekusanywa kutokana na usomaji na usikilisaji wa kina wa nyimbo teule za Mrisho Mpoto. Mtafiti amechagua nyimbo nne zenye matumizi ya jazanda. Mtafiti

alisikiliza kanda za nyimbo teule za Mrisho kisha akayanukuu maneno kwenye daftari. Licha ya kusikiliza kanda za nyimbo teule za Mrisho Mpoto, mtafiti alisikiliza mahojiano mbalimbali ya msanii huyu kwenye vituo mbalimbali vya redio na runinga katika nchi ya Tanzania. Mojawapo cha vituo hivyo ni Tanzania Broadicasting Cooperation (TBC). Nyanjani, mtafiti alitumia hojaji ambazo alizisambaza kwa wahojiwa. Vifaa vilivyotumiwa ni pamoja na daftari, kalamu na hojaji.

### 1.2 **Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data**

Data kuchanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu kwa kuongozwa na maswali na mihimili ya nadharia ya kimtindo. Uchanganuzi ulifanywa kwa kubainisha aina za jazanda, maudhui yanayowasilishwa kupitia jazanda zenyewe na athari za matumizi ya mbinu hii katika kuwasilisha maudhui. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo, majedwali na takwimu. Nyimbo zenye maudhui yanayofanana ziliteuliwa na kuchanganuliwa pamoja na jazanda zilizomo kwenye nyimbo hizo kama ilivyo katika jedwali hili;

| Maudhui | Wimbo | Jazanda |
|---|---|---|
| Upumbavu | Ahsanteni kwa Kuja<br>Sizonje<br>Ktendawili | Ndoto<br>Paka<br>Mifupa<br>Wakati |
| Utu na Mapenzi | Sizonje<br>Samahani Waanangu<br>Ahsanteni kwa kuja<br>Kitendawili | Masomo<br>Milango<br>Mgongo |
| Ufisadi | Sizonje<br>kitendawili<br>Samahani Wanangu | Milango<br>Baraza<br>Sizonje |
| Utamaduni | Samahani Wanangu<br>Kitendawili<br>Sizonje | Mbwa<br>Bidhaa |
| Ukosefu wa Kazi | Sizonje<br>Ahsante kwa Kuja<br>Samahani Wanangu | Bidhaa<br>Dirisha<br>Nyama |

### 4.0 **Matokeo**

Matokeo ya utafiti wetu yalibainisha wazi kuwa nyimbo za Mrisho Mpoto ambazo zinaumbwa katika lugha ya Kiswahili hazieleweki vyema miongoni wa wananchi wa mji wa Kakamega na viunga vyake. Katika mahojiano yake mwanamuziki huyu mwenyewe katika idhaa ya TBC nchini Tanzania, alikiri kuwa alipoanza, alikuwa na mashabiki wachache waliokuwa wakimwelewa. "Nilikuwa na mashabiki wachache sana waliokuwa wakinieleza nilipoanza hii sanaa ila nashukuru kuwa kwa sasa nina mashabiki wachache wengi ambao wanafuatilia kazi hii… ila mie pia ni mmoja wa mashabiki wao hao wanaofuatilia nyimbo hizi." Tulifahamu uelewa wa ufahamu wa nyimbo hizi teule miongoni mwa vijana kutokana na majibu waliyoyajaza katika hojaji walizozijaza. Katukana na matokeo yaliyopatikana,

waliokuwa na ufahamu wa 20% kurudi chini ambayo ni idadi ya wasailiwa 229 ndio walikuwa wengi mno. Ishara kuwa wasailiwa 72 hawazielewi nyimbo za Mrisho.Wanaoelewa nyimbo hizi kwa kiasi 20%-50% ya wasailiwa, ni 78. Ishara kuwa 20% ya wasailiwa ndio wanafahamu nyimbo hizi kwa kiasi hicho.Wanaozielewa kwa kiasi cha 50%-70% walikuwa 30. Ishara kuwa nyimbo hizi zinaeleweka miongoni mwa vijana hawa kwa 8%. Wanaozielewa kwa kiasi cha 70%-100% hawakupatikana miongoni kwa vijana. Ishara kuwa nyimbo hizi hazieleweki zote mingoni mwa wapenzi wanaozisikiliza. Hili lilifichua ukweli kuwa malengo ya mtunzi wa nyimbo hizi yaafikiwi. Wanaozisikiliza, wamesalia tu kupata burudani bila kuelewa maswala ambayo yanaimbwa kutokana na mbinu ya jazanda ambayo imesheheni katika nyimbo zenyewe. Matokeo ya utafiti wetu kupitia hojaji yalikuwa kama yafuatavyo katika jedwali hili;

| Kipimo | Wasailiwa | Asilimia ya Ufahamu |
|---|---|---|
| Chini ya 20% | 229 | 72% |
| Baina 20% - 50% | 78 | 20% |
| Baina ya 50% - 70% | 30 | 8% |
| Baina ya 70% - 100% | 0 | 0 |

## 5.0 **Hitimisho**

Sura hii imetoa utangulizi wa utafiti kwa kufafanua tatizo la utafiti wetu: Jazanda katika Nyimbo za Mrisho Mpoto. Madhumuni ya utafiti na pia maswali ya utafiti yamedhihirika. Jambo jingine ambalo limefanyika ni kubainisha sababu za kiusomi za kuchagua mada inayoyafitiwa. Upeo na mipaka ya utafiti wetu umeshughulikiwa. Pamoja na hayo, misingi ya nadharia ya kimtindo iliyoitumiwa kuchanganua matumizi ya jazanda katika nyimbo husika imeelezwa. Ufafanuzi wa tafsili ya nadharia ya jazanda huku tukieleza waasisi na waendelezaji wake ukitolewa. Mihimili ya nadharia ya jazanda mpya na ufaafu wake katika kuitafiti mada yetu teule imejadiliwa. Mwishowe yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti yameangaziwa na kufafanua umuhimu wake katika tatizo la utafiti. Sura hii inahitimika kwa kujadili njia mbalimbali za utafiti zilizotumiwa kuchanganua matumizi ya jazanda katika nyimbo za Mrisho Mpoto.

## 6.0 **Mapendekezo**

Utafiti huu wetu ukuwa ukiangazia kipengele cha jazanda, wala hatukushughulikia vipengele vingine vya lugha, wahusika wala maudhui katika nyimbo teule za Mrisho Mpoto. Hivyo basi, mtafiti yeyote atakayeona vianya kuhusu nyimbo hizi za Mrisho Mpoto anaweza kufanya utafiti wake. Isitoshe, yeyote anayetaka kufanya utafiti wa mbinu ya jazanda ama mbinu yoyote ama kipengele kingine chochote katika nyimbo za mwanamuziki huyu kwa kutumia nadharia nyingine anaweza kufanya hivyo maana sisi tulijikita tu katika nadharia ya kimtindo.

## Marejeleo

Alifah, R. T. (2015). *Language Style in Michael Jackson's Selected Song Lyrics*. Thesis. State Islamic Institute of Tulungagung.

Anyona, J.K. (2009). *The Challenges of Open and Distant Learning in Kenya's Public Universities.* Nairobi: Dissertation at Kenyatta University.

Booker, M. Keith & Dubravka Juraga (2005) *Bakhtin, Stalin, and Modern Russian Fiction: Carnival, Dialogism, and History*. Westport: Greenwood P.

Buffon, G. (1930). *Buffon 's Discourse on Style.* Paris: Librairie Hatier Publishers.

Chimera, R. na Njogu. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi. J.K.F.

Crystal D. and Davy D. (1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group Ltd.

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English style* New York: Longman group Limited.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Hirschkop, Ken (2001) "Bakhtin's Linguistic Turn." *Dialogism.*

Kasau, M.E. (2013). Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Rose Muhando. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kothari, C.R. (2007). Research Methodology: Methods and Techniques, New Age International Publishers, Mumbai. India .

Lakoff, G. na Johnson, M. (1980). *Metaphors we Live By.* Chicago: Chicago University.

Prince, Gerald (2003). *Dictionary of Narratology*. Lincoln: U of Nebraska P.

Tuki (2000) *English-Swahili Dictionary.* Second Edition. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007); *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi.

Williams, Patrick (2005). "Dialogism." D. Herman et al. (Eds). *Routledge Encyclopedia of Narrative Theory*. London: Routledge, Zbinden, Karine, "Traducing Bakhtin and Missing Heteroglossia." *Dialogism*.

Leech, G. (1969). *A Linguistic guide to English Poetry,* London: Longman Group Ltd.

Leech, G. N. & Short, M. H. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Pros,* New York, Longman Group Ltd.

Leech, G.N & Short, M.A. (1981). *Style in Fiction: A linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London, Longman Group Limited.

Leech, G.N. (1969). *Linguistic Guide to English Poetry.* London: Longman.

Lodge, D. (1972). *20th Century Literary Criticism*. London: Longman.

Macmillian. (1984). English and Western Literature. New York: Macmillian Publishing Company.

Malenya, M. (2008). *Matumizi ya Lugha na Jazanda katika Nyimbo za Jacob Luseno*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mugenda, O. and Mugenda, A. (1999). *Research method. Quantitative and qualitative approaches.* Nairobi: Act Press.

Mungai, M.J. (2014). *Fani katika Nyimbo Teule za Anastacia Mukabwa*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nassiuma, D.K. (2000). *Survey Sampling; Theory and methods*. Nairobi. Nairobi. Nairobi

Putra, M.K.P. (2017). *The Analysis of Language Style in Scorpions's Songs*. Thesis. Malang. Maulana Malik Ibrahim State Islamic University of Malang.

Rajwayi, C. (2009). *Maudhui na Mtindo katika Nyimbo za Msanii Faustin Munishi*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Singleton, R. (1993). Approaches to Social Research. New York: Oxford university press.

Wambua, M.S. (2001). *Mtindo wa Nyimbo za Kakai Kilonzo*. Tasnifu ya M.A Kenyatta University. (Haijachapishwa).

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Istilahi na Nadharia,* Nairobi, Focus Books.

Krejcie, R.V., & Morgan, D.W., (1970). *Determining Sample Size for Research Activities*. Educational and Psychological Measurement.